**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ABDULRAHIM BUSOKA

**Juni, 2026**

**Kahama**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI

**MAWASILIANO YA SIMU**

**Mkuu wa Shule**:
0753062074/0787762710

**Makamu Mkuu wa Shule;**
0789229980/0753206571

EMAIL: *abdulrahimbusokasec@yahoo.com*

**SHULE YA SEKONDARI,**
**ABDULRAHIM BUSOKA,**
**S.L.P 347,**
**KAHAMA.**

**Juni, 2026**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ABDULRAHIM BUSOKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KAHAMA MKOA WA SHINYANGA MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya ……..……

Shule ya Sekondari Abdulrahim Busoka ipo umbali wa Kilometa 07 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, mwelekeo wa barabara ya kahama-Bukoba, usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi **'KAHAMA BUS STAND'** nauli ni shilingi **2,000/=** kwa hice, shilingi **3,000/=** kwa bajaji na shilingi **4,000/=** kwa pikipiki. Muhula wa kuanza Masomo unategemea tamko la serikali, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni ndani ya siku 14 kuanzia tarehe tajwa na serikali.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

## 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni skirt 02 za rangi ya **darkblue green (Channel blue) istimu kitambaa namba 01,** urefu kwenda chini ivuke magoti isiyopungua inchi 7 ikiwa na linda box moja mbele na moja nyuma, malinda matatu madogo pembeni. **(Ili kuepuka kubadilika kwa rangi ya kitambaa angalia Mfano wa kitambaa kabla ya kurudufisha (kutoa copy) fomu ya maelekezo ya kujiunga na shule**

ii. Mashati 02 meupe yenye mikono mirefu.

iii. Kwa waislamu rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. Hijab ya kushindia iwe ya rangi ya light blue.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili ndefu (Stocking) rangi ni nyeupe za shule na soksi nyeusi mbili ndefu kwa ajili ya jioni/Usiku.

vi. Sare za michezo ni track suit, bukta na tisheti yake, (zote ziwe rangi ya blue) pamoja na raba nyeupe

vii. Sweta moja 01 yenye mikono mirefu ya rangi ya kijivu yenye shingo V na michirizi myeupe shingoni na mikononi.

viii. Nguo za kushindia (shamba dress) 02 rangi ni light blue ya mikono mifupi (ya shati), aina ya mshono ni solo.

ix. Tai moja ndefu rangi ya kijivu na mistari myeupe.

x. Tisheti moja ya rangi ya bluu yenye kola na nembo ya shule.

**TANBIHI**: **Viambata vyote vya sale za shule vimeambatishwa kwenye fomu hii**

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Daftari 12

ii. **Ream (A4)** Mbili (2) aina ya **DOUBLE A AU A-ONE** kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

UNASHAURIWA KUJA NA VITABU ANGALAU VIWILI KWA KILA SOMO KULINGANA NA TAHASUSI UNAYOSOMA.

**BIOLOGY:**

A. Comprehensive Biology.
B. Biological Science.
C. Understanding biology.
D. Functional approach.
E. CHAND.
F. Biology for Advanced secondary school TIE

**CHEMISTRY:**

A. Chand XI, XII
B. A-level chemistry ramsden 4th Edition.
C. Conceptual Chemistry.

D. Organic Chemistry part 1, 2.
E. Inorganic Chemistry for A level part 1,2
F. Soil Chemistry
G. Physical Chemistry A – level.
H. CHEMISTRY for Advanced secondary school TIE

**PHYSICS:**
A. Principles of physics. By Nellcon.
B. Principles of physics by chand. Class XI and XII)
C. Roger Muncaster.
D. ABC Modern Physics 1,2
E. PHYSICS for Advanced secondary school BY TIE

**ADVANCED MATHEMATICS**
A. Chand class XI
B. Chand class XII vol. 1
C. Chand class XII vol. 2
D. Pure mathematics one by Back house.
E. Pure mathematics two by back house
F. Advanced mathematics by Tranter
G. Advanced mathematics for Advanced secondary school by TIE

**GEOGRAPHY**
A. An Integrated Regional Study on Human and Economic Geography.
B. Africa In Diagram – By Bunnel
C. Geography for advanced secondary school by TIE

**HISTORY**
A. A Major Event in World History 1,2
B. Mastering History 1,2 C. History of Africa.
c. History for Advanced secondary school by TIE

**LANGUAGE**
A. Advanced Level English "A practical Approach"
B. Advanced learner English Dictionary
C. English for Advanced Secondary Schools student's Book. Form five by TIE

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Godoro futi 2 au tatu
vi. Mashuka pair 2 yenye rangi ya lightblue, blanketi 1, foronya 1, chandarua 1 ya rangi nyeupe pamoja na shuka moja jeupe.
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) na kubwa 1 zenye mifuniko;
x. Vifaa vya USAFI

PCB – Jembe, Mopa, Mfagio mlaini (soft broom) na chelewa.

PCM – Jembe, Mopa, Mfagio mlaini (soft broom) na chelewa.
HGFa– Jembe, Kwanja, reki na chelewa
HGLi - Jembe, Kwanja, reki na sabuni ya maji ya kudekia(Lita 5)
HKL – Jembe, Reki, Mfagio mgumu (hard broom) na sabuni ya maji ya kudekia(Lita 5)
HGL - Jembe, reki, Kwanja, Mfagio mlaini (Soft Bloom)
HGK - Kwanja, Mfagio mgumu (Hard bloom), Mopa, na Chelewa

xi. Mwanafunzi anashauriwa kuja na taa ya mwanga wa jua kwa matumizi endapo umeme umekatika.

xii. Mfuko au begi dogo la kubebea Madaftari na vitabu

xiii. Vifaa vya kujifunzia darasani kama vile kalamu, madaftari, penseli, Mathematical set, Non programmable Scientific Calculator (fx-991MS)

Mengineyo: ***Mafuta ya kubadilisha rangi ya ngozi, mafuta yenye harufu kali (perfum, body spray, Wanja, lipstic pamoja na make up) HAZIRUHUSIWI.***

### 2.3 Michango mbalimbali

**Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **Na. 30610011768** jina **ABDULRAHIM BUSOKA SEKONDARI** katika benki ya **NMB** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye paying slip).

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa wa Baba, mama, mlezi, kaka, na Dada pekee**).
- **Kwa mwanafunzi ambaye ana bima ya afya anashauriwa kuja nayo, kwa ambaye hana anatakiwa kuja na kiasi cha shilingi 50,400/= ili akatiwe bima ya afya awapo shuleni.**

- **Mwanafunzi mwenye tatizo la kiafya anatakiwa kuja na vyeti vya Hospitali vinavyothibitisha tatizo lake.**

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni;
vii. Kufuga ndevu;

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ……………………

**Jina la Mkuu wa Shule; FARAJA W MULESI**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** **………………………………..**




**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0753062074**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0789229980/0753206571**

- ➢ **Mwandamizi Taaluma 0694334757**
- ➢ **Mhasibu wa Shule 0784914677/0754298329**

## MEDICAL CERTIFICATE FORM

To be completed by a government medical officer in respect of form    Entrants.

Student's full name……………………………………………………………..

Blood count (red and white)………………………………………………..

Stool examination…………………………………………………………………

Analysis…………………………………………………………………………………..

Syphilis test…………………………………………………………………………….

Eye test…………………………………………………………………………………….

Ears…………………………………………………………………………………………..

Chest………………………………………………………………………………………….

Spleen…………………………………………………………………………………………

Abdomen…………………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION:** Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases etc.

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

certify that person examined above is fit/unfits for admission into a boarding school.

Signature…………………………………….

Designation…………………………………….

Station……………………………………….

Date…………………………………………

**MAELEZO BAYANA (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)**
**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. jina kamili la mwanafunzi……………………………………………….
2. tarehe ya kuzaliwa…………………………………………….
3. jina la baba/mlezi………………………………….
4. jina la mama………………………………………...
5. kazi anayofanya baba……………………………
6. kazi anayofanya mama………………………………...
7. anuani ya baba/mama………………………….
8. anakilema chochote…………………………………...
9. anapendelea kushiriki michezo gani?......................
10. taja ndugu wasiopungua wanne(4) wa karibu wanaoweza kutoa msaada/kumtembelea mwano awapo shuleni pale inapobidi.

| S/NO | JINA | UHUSIANO | KAZI | NO.ZASIMU |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

**MAKUBALIANO (IJAZWE NA MWANAFUNZI/MZAZI)**

1. Baada ya kusoma kwa makini maelezo, taratibu za sheria za shule. Mimi mwanafunzi (majina)…………………………………………………………….
   sahihi…………………………………..
   naahidi kuwa nitatekeleza kwa vitendo yote yaliyotajwa na kwamba itakuwa kosa kukiuka taratibu kanuni na sheria za shule.
2. mimi (mzazi) ………………………………….. nimesoma sheria na taratibu za shule na nakubaliana nazo na kwamba kama mzazi nitakuwa msitari wa mbele kushirikiana na walimu katika kusimamia malezi, nidhamu na taaluma ya mtoto wangu.

   Sahihi ……………………………

**SHULE YA SEKONDARI ABDULRAHIM BUSOKA**

**KAHAMA**
**SHINYANGA**



**KIAMBATA 1: RANGI YA SKETI**



**KIAMBATA 2: TAI YA SHULE**



**KIAMBATA 3: RANGI YA SWETA**



**KIAMBATA 4: GAUNI LA KUSHINDIA (SHAMBA DRESS)**




**KIAMBATA 5: MUONEKANO WA TISHETI KWA NYUMA**



**KIAMBATA 6: MUONEKANO WA TISHETI KWA MBELE**